CHAPISHO LA UKWELI #3

COVID-19: TAREHE 6 - 12 JULY 2020

TAKWIMU

AFRIKA KUSINI

MAAMBUKIZI YALIYOTHIBITISHWA	224,665
WALIOPONA	106,842
VIFO	3,602

JAMHURI KIDEMOKRASIA YA KONGO

MAAMBUKIZI YALIYOTHIBITISHWA	7,432
WALIOPONA	3,226
VIFO	182

ZAMBIA

MAAMBUKIZI YALIYOTHIBITISHWA	1,895
WALIOPONA	1,348
VIFO	42

IVORY COAST

MAAMBUKIZI YALIYOTHIBITISHWA	11,504
WALIOPONA	5,571
VIFO	78

TANZANIA

MAAMBUKIZI YALIYOTHIBITISHWA	509
WALIOPONA	183
VIFO	21

Chanzo: app.powerbi.com

JE, WAJUA?

Wanawake huchangia 70% ya wafanyakazi katika sekta ya afya na kijamii ulimwenguni kote, na wako kwenye mstari wa mbele wa mapambano na COVID-19. Katika ya sekta ya afya na kijamii, kuna pengo kwa mapato ya jinsia la wastani 28%, ambalo linaweza kuongezeka zaidi wakati wa majanga. Mahitaji wa wafanyakazi wa huduma za afya huzidi vifaa vya kinga vya kibinafsi tu, ila pia hujumuisha afya ya kisaikolojia, afya ya uzazi na msaada wa kudumisha usafi. Majanga ya kimataifa huleta tishio kubwa kwa ushiriki wa wanawake katika shughuli za kiuchumi, haswa wanawake walio katika sekta zisizo rasmi kama za biashara ya kupamba nywele (saluni) au uzaji mboga. Wanawake pia ndio idadi kubwa ya nguvu-kazi ya kinyumbani na ya utunzaji, na familia ambazo hutegemea mapato yao hujipata katika hali magumu nyakati kama hizi. Kumbuka kutumia sauti yako kutetea masilahi ya wanawake na wasichana, kwani ukosefu wa usawa wa kijinsia unadhoofishwa zaidi na janga la COVID-19.

Chanzo: UNICEF

SAUTI ZA VIJANA

REFILOE MORAPEDI (AGANANG FM) - AFRIKA KUSINI

SWALI: ***"Wanasayansi na madaktari wanavyowajibika kupata chanjo ya COVID-19, itakapopatikana, je, itapeanwa kwa kila mtu au ni kwa watu walioambukizwa tu?"***

JIBU: Chanjo imeundwa kulinda watu kabla hawajaambukizwa virusi. Kimsingi, chanjo hutumiwa ili kufunza mfumo wa kinga ya mwili kutambua na kushambulia virusi wakati vinaingia mwilini. Chanjo hulinda mtu ambaye tayari alipata hiyo chanjo, na pia jamii.
Kufikia Mei 11, chanjo nane zilikuwa zikifanyiwa majaribio ya kliniki kwa watu ulimwenguni kote, kwa malengo ya kutambua chanjo inayofaa ya COVID-19. Majaribio ya kwanza ya chanjo ya COVID-19 barani Afrika ilianza mnamo Juni 24 nchini Afrika Kusini.
Chanjo hiyo ilitengenezwa katika chuo cha utafiti cha Oxford Jenner, nchini Uingereza, na kwa sasa inaendelea kujaribiwa humo Uingereza, ambapo washiriki zaidi ya 4,000 tayari wamesajiliwa kwenye majaribio hayo ya kliniki. Chanjo inayotumika katika jaribio la Afrika Kusini ni sawa na ile inayotumika katika nchi za Uingereza na Brazil.

Chanzo: Council On Foreign Relations

MMAKUBU PHOKWANE (MCRS) - AFRIKA KUSINI

SWALI: ***"Je, ni nini kitakachotokea kwa mtu ambaye ana VVU na vipimo vinaonyesha kwamba ana virusi vya korona pia?"***

JIBU: Kwa sasa, hakuna taarifa maalum kuhusu hatari za COVID-19 kwa watu walio na VVU. Wazee na watu wa umri wowote wenye hali duni kiafya wanaweza kuwa hatarini kubwa ya kuambukizwa magonjwa hatari, pamoja na watu ambao miili yao haina kinga ya kutosha. Hatari kubwa iliopo kwa watu walio na VVU sana sana ni kwa:

- Watu waliopungukiwa na seli za kinga za CD4 mwilini, na
- Watu ambao hawatumii dawa za VVU (tiba ya antiretroviral au ART).

Watu walio na VVU pia wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya kupitia makali ya ugonjwa wa COVID-19 kulingana na umri wao na hali zingine za kiafya.

Chanzo: Centers For Disease Control and Prevention

ANNIE SAKALA - (FLAVA FM) KITWE, ZAMBIA

SWALI: ***"Kadiri idadi ya kesi za korona zinavyozidi kuongezeka, ni hatua zipi zilizowekwa kwa wanawake tunapofikia suala la upatikanaji wa huduma za upangaji uzazi? Watazipataje iendapo taifa litafungwa kwa muda ili kuzuia maambukizi kuenea (lockdown)?"***

JIBU: Utafiti uliofanywa na Umoja wa Mataifa unaonyesha athari ambayo COVID-19 inayo kwenye mifumo ya afya kwa kuweka vizuizi kwa huduma ambazo zinapaswa kutolewa kwa wanawake na wasichana. Hii inamaanisha kwamba wanawake na wasichana wengi watakosa kufika kwenye vituo vya huduma za afya wakihofia kuambukizwa Covid-19. Minyororo ya usambazaji bidhaa ya ulimwengu pia inaweza kuvurugika wakati wa kufungwa (lockdown), na kunaweza kuwa na uhaba wa mbinu za upangaji uzazi.
Mifumo ya afya inapokuwa imejaa, nchi zinahitaji kufanya maamuzi magumu kusawazisha mahitaji yaliopo ya COVID-19, na pia kudumisha utoaji wa huduma zingine za afya.
Serikali kote ulimwenguni zinapaswa kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma za upangaji uzazi na haki za utunzaji wa afya ya kijinsia na uzazi zimeheshimiwa, hata COVID-19 ikiwepo. Upatikanaji wa mbinu bora za upangaji uzazi ni njia mojawapo ya kupunguza gharama kubwa ya vifo vya kina mama kwa kuzuia ujauzito usiotarajiwa, na kulinda afya ya mwili na akili.

Chanzo: Shirika la Afya Duniani

ZINTLE MAYABA (COSAT) - AFRIKA KUSINI

SWALI: ***"Swali kuu ambalo wanasayansi wanajaribu kujibu ni kama kilele cha korona kitakuwa wakati wa msimu wa baridi na kupungua ifikiapo wakati wa msimu wa joto, kama inavyokuwa na homa. Tunapaswa kutarajia yapi msimu wa baridi utakapofika? Hali baridi ya hewa itaangamiza juhudi zetu za kutokomeza virusi?"***

JIBU: Kuna misimu tofauti ya virusi vingi. Virusi vya homa na baridi huwa na kilele chake katika miezi ya msimu wa baridi, kisha kupungua wakati hali ya hewa inavyozidi kugeuka kuwa joto. Katika miezi ya msimu wa baridi, watu wanaweza kukaa ndani ya nyumba zaidi, na hivyo kuongeza uwezekano wa watu walio katika hatari ya kuambukizwa na mtu ambaye anamaabukizi nyumbani. Virusi huenea kupitia matone ya kupumua ambayo husambaa wakati mtu aliyeambukizwa anakohoa au kupiga chafya. Na matone yanaweza kuenea zaidi katika hali fulani. Matone hukaa hewani wakati hewa ni baridi na yenye ukavu. Wakati hewa ina unyevu na joto, matone huanguka chini upesi na basi kufanya maambukizi kuwa ngumu. Lakini tukizingatia ukosefu wa uhakika uliopo kwa sasa, maafisa wa afya ya umma wanasema ni lazima tu wapangie yasiyotarajiwa kwasababu kuna uwezekano wa mlipuko kuendelea kuenea kwa hali yoyote ya hewa.

Chanzo: Goats and Soda (NPR)

GRACE CHABU - (FLAVA FM) ZAMBIA

SWALI: ***"Kulingana na kampeni za barokoa (maski), je, zinapaswa ziwe nyembamba au nzito ili ziweze kutupatia ulinzi mzuri?"***

JIBU: Ingawaje barokoa (maski) iliyotengenezewa nyumbani haifikii usawa wa zile maarufu za N95, kuwa na kitu cha kujikinga usoni kunaweza kusaidia kuzuia chembe chembe kadhaa zilizo hewani - na hiyo ni muhimu katika juhudi za kuzuia maambukizi ya COVID-19. Utafiti unaonyesha kwamba kuna vitambaa vilivyo bora kuliko vingine inapofikia uwezo wao wa kuwa 'vichungi' vya kuzuia upitaji wa chembe chembe. Barokoa (maski) iliyotengenezewa na tabaka mbili za kitambaa kizito cha pamba, (kitambaa chenye hesabu ya nyuzi angalau 180) ni bora zaidi. Nyenzo bora na iliyopendekezwa ni zile nene za pamba - na ingawa unaweza ukakosa kuwa na kitambaa cha aina hii nyumbani, bado unaweza tu kutumia kitambaa kingine chochote kizito cha pamba ambacho utaweza kupata. Unaweza pia kutumia t-shati, kitambaa cha kufuta kamasi, au vitambaa vingine vyovyote ambavyo vinavyoweza kufuliwa ili kujitengenezea barokoa yako. Hata ikiwa haifikii kiwango cha ubora wa juu zaidi, bado itasaidia pakubwa kukukinga dhidi ya kuambukizwa virusi.

Chanzo: Live Mint